The Church of Lutherany Confession in the Congo

Église Luthérienne de Confession au Congo

« ELCC »

Kanisa la Kiluther la Ungamo Congo

# LITURGIA YA KANISA

TUMWABUDU MUNGU WETU

*Ps 26 :6-8*

*Ps6 :3*

# Utangulizi

Wa pendwa wa Kristo na wachungaji wa kanisa la kilutheri ungano Congo, tuna Shukuru leo hii kwa kupata liturgia ya kanisa, ambayoi kwa muda mefu tulikuwa tukisaidia ma liturgia ya muda ulito lewa na kanisa mbele, hasa tuna wapatia pongezi viongozi wetu kanisa, hata kundi la traduction uliojetolea kwa kufanya kazi ile ya kwanza na ya pili

Shukrani yetu pia iwaendee wa Missionnari wetu hasa ; Pastori Bruce Naom, Pastori David Koenig, kutoka kanisa dada la amerika, na Pastori Mutombo Muzakuza
Ombao walijitoleo kutuletea liturgia hii, tunashukuru kwa Baba representant wetu alie kubali tufanye kazi ya kutafisiri liturgia hii, ili tusifu mungu pamoja na ndugu zetu wa mahali pote ulimwenguni. Kama vile mwinbaji anasema katika zab 26:7,8 heri kukao katika ngumba ya bwana. na kupeleka sauti ya sifa

## YALIYOMO (tableau de matière)

Liturgia.........................................................................

1. Ibada ya siku ya bwana (dimanche........................)
2. Ibada ya meza ( saint scene )................................)

1. **<u>IBADA YA SIKU YA BWANA</u> ( Dimanche )**

- ibada longozwe na Pasteur ao mzee wa kanisa

**OMBI LA UKIMYA**

- **Mchg** ombe ombi la ukimya mbele ya altare na kukaa wimbo – Cantiques

**<u>Kiingilio na ombi</u>**

- **Mchg** : **Kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu.** *Math 28 :19 6*

**Wote** : Utukufu uwe kwa Baba
Utukufu uwe kwa Mwana,
Utukufu uwe kwa Roho Mtakatifu, Amin

**Wimbo**

**Mchg** :

Wapendwa wa Bwana huu ni wakati wa kupatana na mungu wetu tuondoshe mawazo yoyok mabouya.

- Maelezo mafupi kwa nwenendo ya ukisto

**Mchg**: tumukaribishe Mungu wetu katika utatu mtakatifu:
Bwana nani atakaye kaa katila hema yako?
Nani atayepanda katika mlima wako

Mtakatifu?

Mwenye kutemea kwa haki, na kutenda haki anayesema kweli moyoni mwake. Yeye Asiyesingizia kwa ulimi wake, wala hatendei na fiki yake mabaya, wala halaumu jirani yake.

Machoni mwake mwovu ana zarauliwa. Lakini ana wa heshimu wale wanaogopa Bwana. Yeye anayeapa kwa hasara yake mwenyewe wala hageuki. Hatoi mali yake kwa kula riba. Wala hapokei rushwa amuharibu yeye asiye na kosa, mwenye kutenda maneno haya hayaondoshwa milele Amin.

*Ps: 15*

(**Kama ni meza ya Bwana au siku kuu ya kanisa letu Mchg: asome Amri kumi**)

**Mchg**: Tumsikie Bwana njinsi anayvotufundisha katika neno lake:

Mimi ni Bwana Mungu wako. Usiwe na miungu mingine ila mimi.

Usilitaje bure jina la Bwana Mungu wako.

Ikumbuke siku ya Bwana ulitakase.

Waheshimu baba yako na mama yako

Usiue.

Usizini.

Usiibe.

Usi mshuhudie jarani yako uongo.

Usitamani nyumba ya jirani yako.

Usitamani mke wa jirani yako wala mtumishi wake, wala ng'ombe wake wala chochote alicho nacho

Amin *Exd 20 :1-17*

- Wimbo

Mchg :

Nikasema : Nitakiri makosa yangu mbele ya Bwana.

*Ps 32 :5-6*

**Wote** : Nawe ulisamehe uovu wa Zambi yangu

*Ps 32 :5-6*

## <u>Ungano la Dhambi</u> (Confession des Péchés)

**Mchg** : Wapendwa katika Bwana, tumkaribie Bwana kwa fungua mioyo yetu na kutubu zambi zetu (Tusimame)

**Mchg** : Unirehemu ee Mungu ;

**Wote** : sawa sawa na wema wako,

Sawa sawa na wingi wa rehema

Zako uzime makosa yangu.

Unihoshe kabisa na wovu wangu na kunisafisha na zambi yangu.

Maana nina juwa makosa yangu na zambi yangu ni mbele yangu daima

Nimekukosea wewe pekee ya na kufanya yaliyo mabaya machoni

Mwako: ili ufulikane kuwa mwenye Haki wakati unaposema, na kuwa safi wakati unapotoa Hukumu.

Tazama, nilumbwa katika hali ya uovu, na katika makosa mama yangu alinichukuwa mimba.

Tazama wewe unataka kweli moyoni, na kwa siri utanijulisha hekima, unisafiche kwa hisopo na nitakuwa safi, unioshe na nitakuwa mweupe kupita theluji.

Unifomye kusikia furaha na shangwe, ili mifupa uliyovunja ifurahi, ufiche uso wako. Usitazame Zambi

maovu yangu yote. Umba moyo safi ndani yangu Ee Mungu, na ufanye upya Roho nzuri yangu. Amin

*Ps 51 AO*

**Mchg**:

II Mungu mwenye uwezo, Baba wa Rehema;

**Wote**: Nakiri mbele yako, mimi maskini na mudhaifu wa zambi, maovu yangu yote na zambi. Ile nimekukosea weye, nastahili hasira na Adhabu kwa wakati hii na hata milele.

Naungama kwa moyo wangu wote, na najuta kweli kwa kufanya mabaya, nakushi kwa nema yako isio kuwa namwuisho na kwa mateso yako makali, na kifo chako kisio na kosa, Mwana Mpendwa Yesu Kristo na Bwana wetu, kwa kunipa neema yako na Rehema Amin.

*AO*

III **Mchg:** Mungu Mwenye nguvu, muumba wetu; na Baba yetu, tunakubali na tunakiri kama tulifanya Dhambi mbele yako. Kwa mawazo, kwa maneno hata kwa matendo.

Tumekuja kutafuta kimbilo katika Rehema yako utuhurumie, maskini na wenye zambi na utusamehe makosa yetu katika upendo wa yesu –kristo na bwana wetu.

Utusaidie kwa roho wako mtakatifu kwa kujuwa mapenzi yako matakatifu kwa Neno lako kwa ajili yake Yesu – Kristo Mwana na Mwokozi Wetu Amin.

**IV. Mchg** :

Nakiri hapa mbele ya Mungu, mimi niliye maskini na mwenye Zambi, nimekosea utakatifu kila siku, kwa njia mabli-mbali, si kwa maneno tu wala kwa matendo kwa kukosa huruma, upofu, uono kukosa haki, kasirani, uchafu kwa nmna yote, hata tena kwa Mawazo mabaya, na tama.

Inayo hukumu moyo wangu. Kwa kutoamini kwangu, kiburi, kutamani uchoyo, chuki.

Na kwa mambo mingi ya siri, ambayo ina ni hukumu na Mungu anajuwa mzuri kuliko mimi mwenyewe. Nakataa zambi zangu zote, na naungama, na wiko.

Na uchungu mkubwa juu ya kuifanya, na naomba kwa moyo wangu wote neema ya uhuruma kwa Mungu wangu.

Kwa jina Yesu – Kristo Mwanaa Bwana kunipa nguvu kwa nia ya roho mtakatifu. Amin

**Ondoleo la Dhambi (Absolution des Péchés)**

. **Mchg** : Bwana uturehemu

**Wote** : Kristo uturehemu

**Mchg** : Kristo uturehemu

**Wote** : Bwana uturehemu

**Mchg** : Bwana uturehemu

**Wote** : Kristo uturehemu

***Utukufu ni wa Mungu (Gloria)***

**Mchg** : Utukufu ni wa bwana Mungu

**Wote** : Utukufu we kwa Mungu Juu Mbinguni na Amani Duniani kwa wote wenye moyo mwema.

*Amin – Amin,* *Luc 2 :14*

**Wimbo**

**Mchg** : Bwana awe nanyi

**Wote** : awe Pamoja na roho yako.

*Gal 6:18*

*Phl 4:23*

**Mchg**: **Tuombe (Angalia ombi ya siku)**

**Wote**: Amin

**Wimbo**

**Mchg**: **Tusikie somo letu**

**(Somo kutoka Agano la kale, Lisomue na mzee wa kanisa)**

**Wote** : Oh Mungu wetu, utukufu wako ni mkubwa,

Akuna kiko sawa na weye kwa uzuri, na Mtukufu wako mahali pose macho ya ko inagaa na jina lako lijazwe katika mbingu nadunia.

**Wimbo**

**Mchg** : **(Tusikilize somo letu la waraka) somo kutoka waraka ( epitre lisome wa na mzee xa kanisa)**

**Wote** : Amin Aleluya, Amen Aleluya Amin Aleluya.

- Kama ni wakati wa Majilio na Noeli

**Wote** : Hosana, mbarikina awe Mwokozi anakuja kwetu na mapendo, ana yeshuka kutoka tumbo la Baba,

ubarikiwe Bwana ana kuja juu ya mbingu na kuletea watu wokovu na utukufu.

- **(Wa kati wa mateso) itumike sehemu hii**

  Kandoo aliye umiya kweli, juu ya msalaba ..........................................................................
  ..............................................................................

Una beba mateso yetu, na ulivunja minyororo, Bwana Yesu utufanyie neema.

***Wakati wa Pasaka*** **(maneno hii isemwe wakati wa pasaka)**

Wako utukufu, oh mfufuka, kwako ushindi kwa milele na milele unaangaza nuru, na Malaika alishika akazunguusha jiwe kubwa, ya kaburi ulioshinda.

Kwako utukufu, oh mfufuka, kwako ushindi wa milele na milele!

**Mchg**: Tusikie somo la injili (Evangile)

(Somo la injili lisomwe na mzee moja)

*Luc 11 :28*

Heri wale wanaosikia neno la Mungu na kulichunga (Mzee atasema kiisha somo ili)

**Wote** : Sifa iwe kwako oh Kristo !

**Ukiri wa imani (Credo)**

**Mchg: Tukiri pamoja imani yetu, inayo tupanisha sisi na wakristo wote ulimwen nguni**

**<u>Imani ya mitume</u>**

**Wote**: (Tusimame)

Namwamini Mungu Baba, mwenyezi Muumba wa mbingu na inchi.

Namwamini Yesu Kristo, Mwana wako wa pekee Bwana wetu, aliye chukuliwa mimba kwa uwezo wa Roho mtakatifu, akazaliwa na Bikira, Mariam, akateswa zamani za pontis Pilato. Akasulubiwa, akafa, akazikwa, akashuka kuzimu, siku ya tatu akafufuka kutoka kwa wafu, akapaa mbinguni ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba Mwenyezi, kutoka huko atakuja kuwahukumu walio hai na wafu. Namwamini Roho Mtakatifu, kanisa Takatifu la Kikristo usharika wa watakatifu ondoleo la Dhambi, kufufuliwa kwa muili, na uzima wa milele Amin. (Kukuw)

*AO*

**(<u>Kama ni sikukuu au siku special</u>)**

**Imani ya Nikea**

**Wote** : (Wasimame)

Naamini Mungu moja, Baba Mwenyezi, Muumba mbingu na inchi, na vitu vyote vinavyonekana na visivyoonekana.

Twaamini Bwana moja, Yesu Kristo, Mwana wa Pekee wa Mungu, Mwana wa Azali

- wa Baba. Yu Mungu kutoka Mungu yu nuru kutoka nuru, yu Mungu kweli, Mwana wa Azali
- asiyeumbwa Mwenye Uungu moja na Baba. Kwa yeye huyu vitu vyote vili umbwa.

Alishuka kutoka mbinguni kwa ajili yetu sisi wanadamu na kwa wokovu wetu, akatwaa muili kwa uwezo wa Roho mtakatifu katika Bikira mariamu, akawa Mwanadamu, Akasulubiwa kwa ajili Yetu zamani za Potio Pilato. Aliteswa akazikwa, siku ya tatu akafufuka kamo yasemayo Maandiko Matakatifu.

Akapaa mbinguni, ameketi mkono wa kuume wa baba. Naye atakuja tena kwa utukufu kuwa hukumu walio hai na wafu. Na ufalme wake hauna mwisho.

Tumwamini Roho mtakatifu Bwana Mtoa Uzima, atokaye katika Baba na mwana, anayeabudiwa na kutukuzwa pamoja na Baba na Mwana aliyesemwa kwa vinywa vya manabii.

Twaamini kanisa moja takatifu la kristo na la kimitume. Twakiri ubatizo moja kwa ondoleo la Dhambi. Twatazamia kufufuliwa kwa wafu na uzima wa ulimwengu utakaokuja.

*Amin (kukaa)*

(Azali = wa milele, hakuna na Asili)

**Wimbo**

Kisimama

**Somo la hubiri (lisomwe na siku)**

**Wimbo.**

**<u>Sala kuu ya Maombezi</u> (intercession (prière générale)**

**Mchg** : (Tusimame)

Mwenyezi Mungu Baba wa Rehema umeagiza maombezi ya fanyike kwa ajili ya wote. Twakuomba uongoze

kanisa lako takatifu, lidumu na kukua katika umoja na ushuhuda wake wa kweli katika neno la Mungu.

Ukumbuke hasa kazi ya boardi Missioni uko Amerika na mahali pote na wa missionari wetu wote.

Tunawaombea wote wenye Mamlaka katika inchi yetu ya Congo tukikumbuka (Raisi wetu, mawaziri na magavana na wote wenye mamlaka watawale kwa haki na kweli wote tukae kwa Amani, inchi ipate maendeleo mema katika njia mbali mbali.

Tunawaombea Viongozi wote wa kanisa letu hapa Congo, wa fanya kazi mbali – mbali, Kanisani.

Hasa tukikumbuka Baba Representant, Mapastori wote, mashemashi, na wazee wa kanisa, viongozi wa Makundi mbali mbali.

Uwape nuru ya kweli na uongozi katika kazi yao.

Tunawaombea wote wafanya kazi mbali mbali kanisani, sekalimi, hata wote wenye shida mbali mbali, ugonjwa Na taabu ukumbuke wenye shida za kiroho, naya kimwili, ukumnbuke wanaosafiri, baharini na nchini,

Ukumbuke wajane, na watoto mayatima, mwenye huzuni na wenye shida mbali mbali utujalie Tu ufarahie utukufu wa ufalme wako mbinguni pamoja na wote waliofarik

katika bwana utujalie hayo, Baba kwa ajili yake Yesu Kristo Mwaokozi wetu amin

*1 Timotthée 2:1-3*

**<u>Baba yetu uliye mbinguni</u> (notre père**

**Mchg** : Baba yetu uliye Mbunguni ;

**Wote**: Jina lako litukuzwe;

Ufalme wako uje mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama luko mbinguni.

Utupe leo riziki yetu utusamehe makosa yetu kama sisi tunavyowasamehe waliotukosea.

Usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu na utukufu hata milele. Amin

*Math 6:9-13*

**Wimbo**

**Matoleo**

**Ombi Mchg**

Ee Mungu, mwenye neema na rehema uyapokea matoleo ya watu wako, katika upendo wako uyatume, yalete

matunda ya kiroho, ili ufalme wako uenezwe hapa na popote duhiani kwa yesu kristo mwana wako na bwana wetu

*Amin*

**Wimbo**

**Matangazo**

**Wimbo**

**Baraka ya mwisho**

**Mchg:**

Kwa wale wotu wote weko katika msalabani na wale mwenye kuitwa na yesu kristo bwana wetu ule tuna amini tupate kuishi milele na milele Amin.

**Wote:**

Utukufu uwe kwa Mungu muumbaji wetu,

Utukufu kwa kristo mkombozi wetu utukufu kwa roho mfariji wetu, sifa na utukufu kwa mungu mkombozi

Sala ya kimya

Wimbo wa kutoka inje.

## II IBADA YA SIKU YA BWANA (DIMANCHE) NA IBADA YA MEZA YA BWANA (Sainte scène)

**Mchg**: Aombe ombi la kimya akinamisha kichwa kwa altare na **kukaa**

**Wimbo**

**Kiingilio na ombi**

**Mchg:**

Kwa jina la baba , na mwana, na la roho mtakatifu amin.

**Wote** : Utukufu uwe kwa baba,
utukufu uwe mwana ;
utukufu uwe kwa roho mtakatifu
hata milele na milele amin.

**Mchg**: Bwana awe nanyi

**Wote:** Awe na roho yako

**Mchg**: ombi siku

**Wimbo**

**Somo kutoka agano la kale (lisomwe na mzee moja wimbo)**

**Somo la waraka (epitre) lisomwe na mkristo moja)**

**Wote**: Amin aleluya, aleluya amin aleluya.

**Wimbo**

**Somo la injili (Evangile) lisomiwe na mzee moja akimaliza** kusoma atasema.

Heri wale wanasikia maneno ya Mungu na kuichunga,

*Luc 11:28*

**Ukiri wa imani (credo)**

**Voir ibada ya dimanche (tuangalie)**

**Wimbo**

**Mahubiri ya siku**

**Wimbo**

**Sala ya Maombezi ya siku (prière générale)**

**Mchg** : tusimame na kuisha afanye ombi kuu

**Matoleo ao sadaka ya siku na ombi**

**Wimbo**

**Kusubutisha watu ao kutayarisha**

**Mchg**: ndugu wa kristo huu ni wakati wa sisi kupatane na Mungu katika meza ya Bwana tutoshe mawazo yote mubaya ...

**Wote**: (wasimame)

Mungu umba moyo safi ndani yangu, na ufamye upya roho mzuri ndani yangu mbali na uso wako, usiniondolee usiniondolee, Bwana usiniondolee roho wako mtakatifu

*Psaume 51:12-14*

**Mchg**: Nikasema:

Nitakiri makosa yangu mbele ya bwana,

*Psaume 32:5-8*

**Wote:** nawe ulisamehe uovu wa zambi yangu,

*Psaume 32:5-6*

**<u>Ungamo la dhambi</u> (confession des pêches)**

**Mchg** : Mungu mwenye nguvu, Baba wa rehema,

**Wote** : Nakiri mbele yako, mimi, maskini na mudhaifu wa dhambi, maovu yangu na dhambi yangu yote, ile

nilioyo kukosea nastahili hasira na adhabu kwa wakati hii na hata milele.

Natubu kwa moyo wangu wote, na juta kweli kwa kuifanya nakusihi kwa neema yako isuya na mwisho na kwa mateso yako makali na kifo choka kisio na kosa

Kwa mwanao mpendwa yesu kristo na bwana wetu, kwa kunipa neema na rehema. Amin.

**Mchg**: Bwana uturehemu
Kristo uturehemu
Bwana uturehemu

**Wote**: Bwana uturehemu
kristo uturehemu

**Mchg**: Mnakiri kweli zambi zenu mbele ya Mungu? Na mnahahidi kubadilisha mwenendo wenu, na mnaamini kwa moyo yenu, kama neema pekee ya Yesu Kristo inaweza kusamehe makosa yesu. Bila hata msaada wetu hata moja?

**Wote**: ndio bila msaada wetu, ila wake Yesu Kristo

**<u>Utangulizi wa Ibada ya Meza ya Bwana</u>**

**Mchg**: asimame nyuma ya altare (Mazabahu)

**Mchg**: Bwana awe nanyi

**Wote:** Awe na roho yako

**Mchg**: Inueni mioyo

**Wote**: twaiinua kwa Bwana

**Mchg**: tumshukuru Bwana Mungu wetu

**Wote**: Hii ni kweli tena ni haki

**Mchg:** Hii ni kweli tena ni haki kila saa na kila wakati na kila nafasi kukushufuru Bwana mtakatifu. Mungu wa milele kwa Yesu Kristo Bwana wetu.

Twakutiza na kusifu daima tukiimba:

**Wote**: Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu

Bwana Mungu wa majeshi

Mbingu na inchi zimejaa utukufu wajo, hosiana mbingini

Heri anakuja kwa jina la bwana

*Is 6:3, Luc 19:38*

*Jean 12:36; Ps 118:26*

**Ombi ya baba yetu uliye mbinguni**

**Mchg** : (tusimame)

**Baba** yetu uliye Mbinguni…

**Wote**: Jina lako litukuzwe…

*Math 6:9-13*

**Kubarikia mkate na divai (consécration)**

**Mchg** : Ee baba wa mbinguni, kwa rehema yako ulitowa mwana wako wa pekee yesu kristo, ili wote wanao mwamini wa pate uzima wa milele, utusikie tunapo pokea mkate huu na kikombe hiki kama vile mtoto wako aliyo tuagiza : kula na kunwa, muili na damu yako ya bei kwa wokovu.

**Mchg** : Bwana yesu kristo, usiku ule aliotolewa alitiwaa mkate akamshukuru, akisema twaeni na kuleni wote huu dio mwili wangu na fanyeni hivi kwa kunikumbuka.

Hata kisha kwa, alituaa kikombe akashukuru akawapa akisema kunyeni, kwa maana katika kikombe hiki ni Agano jipya katika damu yangu, na Fanyeni hivi kwa kunikumbuka na kutangaza kifo changu hata wakati nitakaporudia.

*1 cor 11 :24-26*

*Luc 22 :19 -20*

**Wote** : Ee baba, tuna tangaza kufa kwa mwanao, na kufufuka kwake na tunakubali kurudia kwake.

**Mchg** : Mkate tumegao, na vinyo tunywao ni ushiraka wa muili na damu ya yesu kristo.

**Wote** : Mkate ni moja, na sisi tulio wengi tuko muili moja kwa maana sisi tulio wengi tuna pokea sehemu ya ule Mkate moja

*1 Cor 10 :17*

**Wote** : Mwana kondoo wa Mungu unaye ondowa zambi ya dunia, utuhurumie ;
Mwana kondoo wa Mungu, unayeondoa zambi ya dunia, uruhurumie
Mwana kondoo wa Mungu unayeondoa zambi ya dunia utupe Amani yako Amin

*Jean 1 :36*

**Mchg** : Tunawaomba wale waliojitanisha na kutengeneza maisha ili wafike katika meza wanakaribisha kila kitu ni tayari.

**Mchg** : agawie wa Kristo mkate na divai

*Luc 14:23*

**Wimbo**

Baada kuwa kabula ombi

**Mchg**: afanye ombi la kushukinu

**Wimbo**

**Baraka**: **Mchg** (angalia ibada kuu ya juma. (Dimanche)

**Wote:** utukufu uwe kwa Mungu mumbaji wetu,

Utukufu kwa kristo Mkombozi wetu

Utukufu uwe kwa roho mfariji wetu

Sifa na utukufu kwa Mungu Mkomozi wetu Amin

Mwisho wa Ibada hii ya meza ya Bwana